


Yesu anakukaribisha kwake kwa maneno haya: “Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha” (Math 11:28). Huwa inakuwa ni furaha kupokea msamaha wowote, lakini kusikia ya kuwa Yesu mwenyewe anatalika sisi, kumwona Yesu mwenyewe akinyoosha mikono yake kwetu, Mwokozi akitafuta wenye dhambi badala ya wenye dhambi kumtafuta Mwokozi, hii inatia moyo na hakika inafariji.

Bwana ni “mwema na tayari kusamehe” (Zab 86:5). “Hufurahia rehema” (Mika 7:18). Yeye “hapendi mtu yeyote apotee” (2Pet 3:9). Kwa furaha “hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli” (1Tim 2:4). Alilia kwa ajili ya Yerusalemu iliyokataa kutubu (Lk 19:41). “Kama mimi niishivyo”, anasema, “sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; ... ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya, mbona mnataka kufa” (Eze 33:11).

Inawezekana unaamini ya kuwa dhambi zako zinaweza kusamehewa na Bwana Yesu Kristo. Lakini, umesamehewa sasa? Je, umemshika Bwana Yesu Kristo kwa imani na tegemeo, na kupata amani kupitia damu yake ya thamani? Nafsi yako iko kwenye hatari kubwa. Kama ukifa kabla ya dhambi zako kusamehewa utakutana na hukumu ya Mungu, na kuadhibiwa milele jehanamu – BILA TUMAINI.

Na Dr. J. C. Ryle.



**Revival**  
MOVEMENT ASSOCIATION

Tuma kwa:

**Revival Movement Association**  
10 Kinallen Road, Dromara,  
Dromore, BT25 2NL, Northern Ireland  
[www.revivalmovement.org](http://www.revivalmovement.org)

THE FORGIVENESS OF SINS - Swahili

# MSAMAHA WA DHAMBI



# MSAMAHA WA DHAMBI

Ninapotembea katikati ya umati wa watu, ninaona wengine wanatafuta furaha na wengine wapo kwenye biashara – wengine wanaonekana matajiri, wengine wanaonekana maskini. Lakini hakuna mwanaume au mwanamke aliye hai ambaye hapendi dhambi zake zisamehewe, au watahukumiwa milele siku ile ya mwisho. Kujua kuwa unahitaji dhambi zako zisamehewe ni hatua ya kwanza ya kwenda mbinguni. Dhambi ni mzigo na unatakiwa uondolewe kwetu. Dhambi huchafua na lazima zisafishwe. Dhambi ni deni kubwa, ambalo ni lazima lilipwe.

Wapi tunaweza kupata msamaha wa dhambi? Kuna uhakika na njia rahisi, na njia ni kumwamini Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wako. Ni kuitoa nafsi yako yenye dhambi, bila kuzuia chochote kwa Kristo – na kuacha kabisa kuzitegemea kazi zako kwa ajili ya wokovu wako – na kutotegemea kazi nyingine isipokuwa kazi ya Kristo tu, si haki nyingine isipokuwa haki ya Kristo kama msingi wa tumaini lako la uzima wa milele.

Chukua njia hii na utakuwa nafsi iliyosamehewa. Kwa Kristo, Petro anasema, “manabii wote wanamshuhudia ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi” (Mdo 10:43). “Ya kuwa kwa huyo” Paulo anasema kule Antiokia, “mnahubiriwa msamaha wa dhambi; na kwa yeye kila amwaminiye, huhesabiwa haki katika mambo yale yote” (Mdo 13:38,39). “Katika yeye,” anaandika Paulo kwa Wakolosai, “ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani masamaha ya dhambi” (Kol 1:14).

## YESU NDIYE MWOKOZI PEKEE

Bwana Yesu Kristo, kwa upendo mkuu na huruma, alitoa malipo timilifu na kamili kwa dhambi, kwa kifo cha mateso pale msalabani badala yetu. Pale alijitoa mwenyewe kama dhabihu kwa ajili yetu na kuruhusu ghadhabu ya Mungu, ambayo sisi tulistahili, kumwangukia kichwani kwake mwenyewe.

Kwa ajili ya dhambi zetu, kama aliyejitua badala yetu, alijitua

mwenyewe, akateseka na kufa – mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, asiye na hatia kwa ajili ya waovu – ili aweze kutukomboza kutoka katika laana ya sheria iliyovunjwa, na kutoa msamaha kamili kwa ajili ya wale walio tayari kuupokea. Na kwa kufanya hivyo, kama Isaya alivyosema, alizichukua dhambi zetu; na kama Yohana Mbatizaji alivyosema, amezichukua dhambi zetu; kama Paulo alivyosema, ametutakasa dhambi zetu na kuziweka mbali nasi; na kama Daniel alivyosema, amekomesha makosa na kumaliza dhambi.

Toba kwa ajili ya dhambi na kumwamini Bwana Yesu Kristo, ndiyo mambo pekee yanayohitajika kwa ajili yako wewe na mimi kuweza kusamehewa dhambi zetu. Kwamba tunakuja kwa imani kwa Yesu kama wenye dhambi tukiziungama dhambi zetu – kumtegemea – kutulia kwake – kushirikiana – kumkabidhi nafsi zetu kwake – na kuacha tumaini jingine lolote, na kujitua kwake tu – haya ndiyo yote ambayo Mungu anayohitaji. Ukiyafanya hayo utaokoka. Dhambi zako zitakuwa zimesamehewa kabisa, na uovu wako wote kuondolewa.

# MSAMAHA